# 15 VIWANGO VIWILI VYA UPENDO



Hapana nguvu iliyo kubwa kuliko upendo. Ndilo jambo kuu lililopata kuimbwa na kuandikiwa zaidi na washairi. Ndio uwezo wa juu zaidi. 1 Wakorintho 13:13. Watoto wanahitaji upendo wa mama zao. Ndio unaowapatia maisha na kuwasaidia kukua kiafya. Upendo ndio unaomstawisha mtoto na tamanio la vijana. Watu wengi wamejiondolea maisha yao kutokana na mambo ya kukatisha tamaa! Hawakupenda na wala hawakujisikia kupenda. Upendo ndio mfumo mkongwe zaidi katika kumsaidia mwanadamu.

## UPENDO UMEANDIKWA KATIKA DAMU

**1. Je, Mungu aliwaachilia mbali viumbe Wake aliowaumba, licha ya kutokuwa na shukurani kwao? Luka 19:10.**

______________________________________________________________

**2. Mfano mkubwa zaidi wa upendo wa Mungu kwa mwanadamu ulikuwa ni upi? 1 Yohana 4:9-11.**

______________________________________________________________

**3. Je, twawezaje kuwa marafiki wa Yesu na kuonyesha upendo wetu Kwake? Yohana 15:14, 10; 14:15.** ________________________________________

*Hatuwezi kununua mbingu kwa njia ya matendo yetu. Wokovu ni karama ya Mungu (Wagalatia 2:16). Hata hivyo, wokovu ni ule utendaji wa Mungu "katika mwanadamu" kwa njia ya Roho Mtakatifu.*

**4. Iwapo tunataka kufuata mfano wa Kristo, tutendeje ili kuupata wokovu wa milele? Waebrania 5:8, 9.** ________________________________________

**5. Maana halisi ya amri hizi ni nini? Mathayo 22:37-40.**

*Kuna viwango viwili vya* ____________________*. Upendo ni ile nguvu inayokufanya umpende Mungu.*

*Je, ni kwa nini Mungu alimpatia Musa mbao mbili badala ya moja?*

- Katika ule ubao wa kwanza kuna zile amri nne za kwanza, ambazo zinatueleza juu ya namna ya kumpenda Mungu. Huu ndio upendo katika kiwango cha kwanza.
- Katika ubao wa pili, tunakuta amri sita za mwisho, ambazo zinahusu jirani zetu. Hiki ni kiwango cha pili cha upendo.

## UPENDO KATIKA KIWANGO CHA KWANZA

**6. Tunaonyeshaje upendo wetu kwa Mungu kwa kulingana na amri tatu za kwanza? Kutoka 20:3-7.**

a) Kumweka Mungu katika mahali pa kwanza; zaidi ya mambo yetu yote yanayotufaidia ya kidunia, majisifu yetu, heshima zetu binafsi, n.k.

b) Tusimwabudu kama vile tuonavyo sisi bali kama alivyoagiza Yeye, katika roho na kweli.

c) Tukilichukulia jina Lake kwa heshima na kicho.

**7. Tunaoneshaje upendo wetu kwa Mungu pale tunapoitunza Sabato? Kutoka 20:8-11.**

*Kwa kuziratibu kazi zetu za juma tangia siku ya kwanza ya juma ili kwamba tuweze kuiweka kando siku ya saba mahususi kwa Mungu. Tunakumbuka kwa shukurani juu ya kazi ya uumbaji wa Mungu kwa njia mbili (Zaburi 118:24):*

***Kimwili:*** *kufurahia amani katika siku ya pumziko kwa kuwako katika mazingira ya asili.*

***Kiroho:** kufurahia lile badiliko Kristo alilolifanya ndani yetu. Haipasi kuwa ni pumziko la kimwili tu bali ni pumziko ambamo Kristo, Mwanzilishi na Bwana wa Sabato, anakuwa ni pumziko letu la kiroho kwa njia ya kazi Yake ya kutuhesabia haki (Waebrania 4:1, 2, 9, 10). Kila Sabato yapasa kuwa kionjo cha mbele cha uzima wa milele.*

**8. Sabato huanza na kwisha lini? Biblia inaiitaje ile siku ya sita?**

*a) Kwa kulingana na Biblia, siku huanza pale jua linapozama. Walawi 23:32; Nehemia 13:19.*
*b) Ijumaa, siku ya sita, inaitwa siku ya maandalio. Marko 15:19.*

***Kina mama wa nyumbani pia wastahili pumziko, hivyo wanapasa kufanya nini katika ile siku ya maandalio? Kutoka 16:23.** Maadamu ni siku halisi ya maandalio, tunapasa kununua kila kitu kinacho-hitajika, kusafisha nyumba, kuoga na kubadili nguo, na kuweka kando mavazi yatakayotumika Sabato.*

**9. Je, ni jinsi gani ambavyo Bwana anataka tuitunze ile anayoiita kuwa ni "Siku ya Utakati-fu Wangu"? Isaya 58:13, 14.**

____________________________________________________________

a) Kutofanya ________________________, yaani kutofanya biashara zo zote, ama kujitia wenyewe katika majukumu mbali mbali, pamoja na starehe, n.k.
b) Kutosafiri pasipo lazima isipokuwa katika kumtumikia Bwana.
c) Kuto_________________________ juu ya matatizo ama vitu vinavyoonekana. Kutosoma magazeti ama kusikiliza habari. Inapasa kuwa ni siku takatifu hasa iliyowekwa kando kwa ajili ya Mungu.
d) Tusifanye mambo ambayo yatawafanya watu wengine watutendee sisi kazi (Kutoka 20:10).

**10. Iwapo tunampenda Mungu, ni majibu gani tutakayoyatoa kwenye vipingamizi vifuatayo?**

a) Kwani siku zote sio sawa? Kutoka 20:11; Mithali 16:25. Mungu alistarehe, akaitakasa na kuibariki siku hii maalumu.
b) Watu wengi huiadhimisha Jumapili. Je, mamilioni haya ya watu wanaweza kukosea? Mathayo 7:13, 14.

   Suala husika sio kama tunasimama upande wa walio wengi ama walio wachache, bali ni iwapo tupo upande wa Yesu.
c) Wazazi wangu na kina babu walitunza Jumapili, nami sipendi kuwa tofauti. Matendo 17:30. Mungu husamehe dhambi zote zilizokwisha tendeka kutokana na kutofahamu (Yakobo 4:17).

**11. Iwapo tunampenda Yesu, tutafanya nini katika siku Yake? Luka 4:16.**

*Yesu alikuwa na desturi ya* ____________________________________________

*a) Tunapasa kuhudhuria ibada za kidini ili kumwabudu na kusikiza neno Lake.*
*b) Twaweza kuwatembelea wagonjwa na kupoza maumivu yao (Mathayo 12:11, 12).*
*c) Twaweza kuongea na watu wengine juu ya habari njema ya wokovu.*

## *TWAWEZAJE KUPENDA KATIKA KIWANGO KILE KINGINE?*

**12. Zile amri sita za mwisho zinawahusu jirani zetu. Tunauoneshaje upendo wetu kwao?**

a) Amri ya tano inahusu mahusiano kati ya wazazi na watoto wao (Waefeso 6:1-4).
b) Iwapo ninampenda jirani yangu, naweza kumwua? Naweza kuchukua silaha vitani na kuua wingi wa watu? Naweza kutokuwa mwaminifu kwa mwenzi wangu? Je, naweza kusema mambo mabaya juu ya jirani yangu, uongo, kuiba, ama kutamani kitu chake (Warumi 13:9)?

**13. Iwapo upendo ndio msingi wa maisha yetu, je, itakuwa ni vigumu kuishika ile sheria ya Mungu katika viwango hivi viwili? 1 Yohana 4:20, 21; 5:2, 3.**

____________________________________________________________

**14. Je, ni kitu gani ambacho hatuwezi kukisahau iwapo tunaongozwa na upendo? Yakobo 1:27.**

____________________________________________________________

**15. Je, ni kitu gani ambacho hatuwezi kukipuuzia iwapo tunawapenda kiukweli jirani zetu? Marko 15:9; Zaburi 16:12-14.**

____________________________________________________________

## *HITIMISHO*

Kupenda kunatufanya sisi kuwa na furaha! Tunabarikiwa zaidi tunapotoa kuliko kupokea (Matendo 20:35).

Upendo sio hisia pekee bali ni kanuni ya maisha. Upendo unatufanyna sisi kuwa wastahimilivu, wenye kusamehe, wanyenyekevu na waaminifu kwa Mungu pamoja na jirani zetu (1 Wakorintho 13).

Matokeo ya kuishi katika viwango hivi viwili kwa kila siku, tukimtii Mungu na sheria Yake, ni ufunguo wa mafanikio na furaha yetu (Kumbukumbu 28:1, 2).

Kristo amefanya kila kitu kwa ajili yangu. Nami nimpe kitu gani?

***Uamuzi wangu:*** *Ninakubali ya kwamba upendo wangu kwa Mungu pamoja na jirani yangu huonyeshwa katika kuzishika zile amri za ile Sheria Takatifu.* ○ *Ndio* ○ *Hapana*